JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

## SHULE YA SEKONDARI MILUNDIKWA

JUNE 2024

RUKWA



Edit with WPS Office

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS – TAMISEMI

Mkuu wa Shule:0765885667

Makamu Mkuu wa Shule:0765663057

Matron/Patron:0752227218

Shule ya Sekondari:MILUNDIKWA

S.L.P 634 SUMBAWANGA

Tarehe 30/04/2024

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi

……………………………………………..

S.L.P ……………………………………..

…………………………………………….

Yah: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MILUNDIKWA, HALMASHAURI YA NKASI MKOA WA RUKWA, MWAKA 2024

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024 na atasoma tahasusi ya ………..

Shule ya **sekondari Milundikwa** ipo umbali wa kilometa 50 Kaskazini Magharibi mwa mji wa **Sumbawanga**. Usafiri wa basi kutoka mjini Sumbawanga unapatikana katika kituo cha mabasi **KATUMBA** kwa nauli ya **sh.4000/=,** Au kwa kutumia gari ndogo zinazoanzia **POSTA SUMBAWANGA MJINI** nauli **Tsh 5000** mpaka kijiji cha **KASU** shule ilipo,kwa wanaotokea barabara ya Mpanda-Sumbawanga nauli ni Tsh 14,000/=.Wanafunzi wanaotokea Mpanda, washuke kijiji cha Kasu ndipo shule ilipo. Shule ipo **km 1** kutoka stendi ya Kasu.Nauli ya **BODABODA** ni **Sh 1000** kutoka stendi mpaka shuleni.



Edit with WPS Office

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **1/07/2024**, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **1/07/2024** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **31/07/2024**

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni **KAKI(1)** **NA DARK BLUE (1)** Maelezo ya mshono Picha





ii. Mashati. **MASHATI MEUPE YA MIKONO MIREFU MAWILI**

iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni **NYEUPE** ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama ;

iv. Sare ya Michezo ni track suit ya: **DARK BLUE**

v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

vi. Soksi jozi mbili nyeupe

vii. Sweta **DARK BLUE**

viii. Raba nyeupe (snickers) za michezo



Edit with WPS Office

ix. Nguo za kushindia Rangi ya pink yenye draft ndogo kama PICHA inavyo onesha



x. Tai za **KAKI(1) NA DARK BLUE (1)**

xi. Tisheti (T-shirt) **DARK BLUE** zenye kora ya Dark Blue na nembo ya shule,zinapatikana shuleni kwa bei ya Tsh 15,000/= kwa atakayehitaji.

**Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:**

i. Madaftari **7** counter book **3 QUIRE**
ii. **Ream (A4)** photocopy paper Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika
iv. Scientific Calculator Kwa wanao soma Geography
v. Godoro futi mbili na nusu (2.5 ft kwa 6 ft)
vi. Hakikisha unamleta mwanafunzi akiwa na bima ya afya ya NHIF.
vii. Mashuka ya light blue Jozi 2, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1
viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xi. Vifaa vingine katika mgawanyo ufuatao
    1.Mwanafunzi mchepuo wa **HKL** aje na jembe na mpini wake pamoja na mifagio (2) ya ndani na nje
    2. Mwanafunzi mchepuo wa **HGL** aje na reki moja na mpini wake na mifagio (2) ya ndani na nje
    3. Mwanafunzi mchepuo wa **HGK** aje na kwanja moja na mifagio (2) ya ndani na nje

4.Mwanafunzi mchepuo wa **HGFa** aje na mopa (2) na mipini yake na fagio(1) ya ndani.



Edit with WPS Office

2.2 **Michango mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB: Malipo yote yafanyike kupitia benki, NMB akaunti namba 62001100049 MILUNDIKWA SECONDARY SCHOOL na uje na pay in slip ya benk.**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya



Edit with WPS Office

daktari; na

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

MUHIMU:

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.



Edit with WPS Office

4. **Viambatisho na Fomu Muhimu**

   i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
   ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
   iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
   iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

VINJE .I MWASALA (MKUU WA SHULE)

[redacted]

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule ……………… 0765885667**
- **Makamu Mkuu wa Shule …..0765663057**
- **Mwandamizi Taaluma ………0764744941**
- **Mwandamizi Malezi …………0752227218**



Edit with WPS Office

SHULE YA SEKONDARI MILUNDIKWA

FOMU YA KUKIRI KUKUBALI SHERIA ZA SHULE.

A. SEHEMU YA MWANAFUNZI.

KIAPO CHA UTII:

MIMI ………………………………………………………………

Nikiwa mwanafunzi wa Shule hii nakubali kuwa, umma wa nchi hii ya Tanzania ndiyo ulionipa nafasi hii maalumu ya masomo, ili nimalizapo niweze kulitumikia Taifa na kuleta Maendeleo.

Hivyo basi ninaahidi kwamba, nitajibidisha hapa shuleni na pia nimalizapo shule. Ili kutimiza shabaha hiyo ninakubali na kuahidi kwa hiari yangu mwenyewe kuwa nitatii sheria za shule na amri zote nitakazopewa na walimu wangu.

Nikiwa na malalamiko au maoni nitayafikisha kwa viongozi wa shule kufuatana na utaratibu uliowekwa bila ya kuongeza chochote. Nitakuwa tayari kuchukuliwa hatua za kinidhamu zinazostahili iwapo nitakuwa nimekiuka sheria za shule.

**Sahihi ya mwanafunzi ------------------------------------ tarehe ---------------------------- SEHEMU YA MZAZI/MLEZI**

Mimi ………………………………………………… ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi mtajwa hapo juu, naahidi kutoa ushirikiano mzuri na uongozi wa shule katika kumlea mwanangu. Hii ikiwa ni pamoja na kutomruhusu mwanagu kuja na simu shuleni. Nitakuwa tayari kushirikiana na uongozi wa shule katika suala la nidhamu ya mwanafunzi na kwamba nitakuwa tayari kukubaliana na adhabu itakayotolewa iwapo mwanafunzi atakuwa amehusika na utovu wa nidhamu.

Sahihi ya mzazi/mlezi ……………………………………………………………………….

Namba ya simu ya mzazi/mlezi …………………………………… Tarehe: ……………

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.





Edit with WPS Office

MKUU WA SHULE

[redacted]

**MINISTRY OF EDUCATION SCIENCE, TECHNOLOGY AND VOCATIONAL TRAINING**

MILUNDIKWA SECONDARY SCHOOL,
P.O. BOPX 634,
SUMBAWANGA.
**RUKWA.**

MEDICAL OFFICER,
---------------------------
---------------------------
---------------------------

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.**

Please examine the above named as to His/Her fitness to is/her fitness as indicated below. Arrange for necessary treatment so that the certificate may be signed and brought to school by the student.

This certificate must be signed by a qualified Medical Officer of recognized hospital.

**MEDICAL CERTIFICATE**

I have examined the above named student with regard to:

**Skin: ------------------------------------**
**Eyes: -----------------------------------**
**Teeth: -------------------------------**
**Spleen: -------------------------------**
**Any disabilities: --------------------**

**Abdomen: -----------------------------------**
**Urine: ------------------------------------------**
**Hemoglobin: -------------------------------**
**Chest: -----------------------------------------**

I Consider that: --------------------------------------------------------------------- He/She is in good health free from infections diseases, and fir to come to school He/She is fit to come to school after having: ------------------------------------------------------------------------- Treatment for: -----------------------------------------------------
She/is not pregnant.

**MEDICAL OFFICER SIGN & STAMP ……………………………………. DATE ……………**



Edit with WPS Office

Edit with WPS Office